**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE**

**015/1** **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1**

(For Both School and Private Candidates)

**Muda: Saa 3** **MAJIBU** **Mwaka: 2018**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D zenye jumla ya maswali matano.

2. Jibu maswali yote

3. Kila swali lina alama 20

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

*Prepared by: Maria Marco for TETEA*

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Katika elimu ya Hadithi, "Mutafakun alayhi" hutumiwa kwa maana gani?
A Hadithi mashuhuri
B Hadithi iliyopokelewa na maimamu wote wa Hadithi
C Hadithi inayopatikana katika kitabu cha Imam Bukhari na Muslim
D Hadithi isiyojulikana wasimulizi wake
E Hadithi iliyosimuliwa na Makhalifa wanne wa Mtume (s.a.w).
Jibu: C
Sababu: "Mutafakun alayhi" inahusu Hadithi zinazopatikana kwa pamoja katika Sahih Bukhari na Sahih Muslim.

(ii) Kazi kubwa ya Sunnah na Hadithi katika maisha ya mwanadamu ni
A kuchambua na kufafanua waziwazi Qur'an tukufu
B kuelezea maisha ya maswahaba
C kuelezea sifa za Mtume (s.a.w)
D kufahamisha maovu waliyokifanya wakafiri wa Waislamu
E kufundisha usomaji wa Qur'an.
Jibu: A
Sababu: Sunnah na Hadithi zinaeleza, kufafanua na kutekeleza mafundisho ya Qur'an katika maisha ya kila siku.

(iii) Mwandishi mashuhuri wa Hadithi katika kipindi cha Tabi'ina alikuwa ni
A Imam Ahmed
B Imam Abu Daud
C Imam Muslim
D Imam Bukhari
E Imam Malik.
Jibu: E
Sababu: Imam Malik alikuwa mmoja wa wanazuoni mashuhuri katika kipindi cha Tabi'ina na aliandika kitabu mashuhuri cha Al-Muwatta.

(iv) Al-Muwatta ni kitabu mashuhuri cha Hadithi kilichoandikwa katika kipindi gani?
A Makhalifa wanne waongofu
B Tabi'ina
C Tabi' Tab'ina
D wakati wa uhai wa Mtume (s.a.w).
Jibu: B
Sababu: Kitabu cha Al-Muwatta kiliandikwa wakati wa kipindi cha Tabi'ina kwa juhudi za Imam Malik.

(v) Aina kuu mbili za Hadithi ni
A Hassan na Dhaifu
B Nabawiyyah na Sahihi


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

C Nabawiyyah na Qudusy
D Hassan na Mutawatir
E Dhaifu na Ahad.
Jibu: D
Sababu: Hadithi imegawanyika katika Mutawatir na Ahad kulingana na idadi ya wapokezi.

(vi) Maana ya Sunnah kisheria ni
A jambo unalopata thawabu ukilifanya na hupati dhambi ukiliacha
B mafundisho ya maswahaba wa Mtume (s.a.w)
C maelezo kuhusu historia ya Uislamu
D matendo ya Mtume (s.a.w) ambayo ni sehemu ya utume wake
E mwenendo au mila.
Jibu: D
Sababu: Sunnah ni matendo, maneno au maelezo ya Mtume (s.a.w) yanayohusiana na dini na utume wake.

(vii) Mtume (s.a.w) amesema: "Mwenye kutubia kabla jua halijachomoza upande wa magharibi, Allah (s.w) atamkubalia toba yake". Hadithi hii inatufunza kuwa
A kuleta toba ni jambo la hiari kwa waumini
B Allah (s.w) hukubali toba wakati wa mchana
C Allah (s.w) husamehe waja wake wakati wa kuchomoza jua
D ni wajibu kuleta toba pale tu mja anapokosea
E toba inapaswa kufanywa kabla ya dalili za mwisho wa dunia.
Jibu: E
Sababu: Hadithi hii inasisitiza umuhimu wa kutubu kabla ya dalili za mwisho wa dunia, kama kuchomoza jua Magharibi.

(viii) Miongoni mwa matukio yaliyoonyesha umuhimu wa kuzitumia Hadithi za Mtume (s.a.w) ni
A mzozo kuhusu nani awe kiongozi wa Waislamu baada ya kutawafu Mtume (s.a.w)
B Sayyidina Omar (r.a) alipokata kuigwa mgawanyo wa zakat
C kuchanganyikiwa kwa Sayyidina Omar (r.a) baada ya kupokea taarifa ya kutawafu Mtume (s.a.w)
D kutofautiana kwa maswahaba kuhusu usomaji wa Qur'an
E kutofautiana kwa maswahaba kuhusu mahali gani azikwe Mtume (s.a.w) baada ya kufariki kwake.
Jibu: E
Sababu: Kutofautiana kuhusu maziko ya Mtume (s.a.w) kulihitaji Hadithi kuleta mwafaka wa kiibada.

(ix) Ni Sahaba yupi anayefahamika kwa umahshuri wake wa kuhifadhi Hadithi nyingi za Mtume (s.a.w)?
A Abu Hurayra
B Sayyidina Abubakar (r.a)
C Sayyidina Omar (r.a)
D Sayyidina Othman (r.a)
E Sayyidina Ali.
Jibu: A
Sababu: Abu Hurayra alihifadhi idadi kubwa zaidi ya Hadithi kuliko sahaba yeyote.

(x) Katika elimu ya Hadithi, "takriri" hutumika kuonyesha
A vitendo alivyokuwa akivifanya Mtume (s.a.w) kila siku
B jambo lililofanywa mbele ya Mtume (s.a.w) alilikisia na hakulikataza
C maneno aliyoyasema Mtume (s.a.w) mwenyewe
D vitendo vilivyofanywa na maswahaba wa Mtume (s.a.w) kila siku
E Hadithi inayoelezea makosa yaliyokuzwa yakirudiwa kufanywa sana na maswahaba wa Mtume (s.a.w).
Jibu: B
Sababu: "Takriri" inahusu matendo yaliyofanywa mbele ya Mtume (s.a.w) na akakubaliana nayo kimya kimya.

2. Oanisha Aya za Qur’an zilizopo katika Orodha A na maelezo ya aya hizo yaliyopo katika Orodha B. Andika herufi ya jibu sahihi kutoka Orodha B pembeni ya namba kutoka Orodha A katika kijitabu chako cha kujibia.

Orodha A
(i) Hayakuwaha haya anayoisema ila ni wahyi uliofunuliwa kwake. Amefundisha Malaika mwenye nguvu sana mwenye uwezo (53:4 - 5).
(ii) Wala si kauli ya mtunga mashairi (kama mnayosema). Ni machache sana mnayoamini (69:41).
(iii) Hiki ni kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake, ni uongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu (2:2).
(iv) Nyinyi mna dini yenu na mimi nina dini yangu (109:6).
(v) Akawafanya kama majani yaliyoila na yakatapikwa (105:5).
(vi) Ni mwenye kuleta baraka (kweli kweli) yule aliyeteremsha Furqan kwa mja wake, ili awe mwongozi kwa walimwengu wote (25:1).
(vii) Na wanakuuliza habari za roho. Sema Roho ni jambo lililohusika na Mola wako. Nanyi hamkupewa katika elimu ila kidogo tu (17:85).
(viii) Bila shaka tunajua kwamba wanasema kuwa yuko mtu anayemfundisha (16:103).
(ix) Soma kwa jina la Mola wako aliyekuumba (96:1).
(x) Hakika tumeiteremsha (hii Qur'an) katika usiku wa cheo (97:1).
(xi) Pana wanaume mikononi mwa Abuu Lahab! Naye amekwisha angamia (111:1).
(xii) Kwa yakini shetani ni adui yenu; basi mfanyeni adui kwani analiita kundi lake liwe katika watu wa motoni (35:6).
(xiii) Ewe Mtume kwa nini unaharamisha alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu? Unatafuta radhi za wake zako... (66:1).
(xiv) ...hatasema siku hiyo ila yule ambaye mwingi wa rehema amempa idhini na atasema yaliyo sawa (78:38).
(xv) Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni mmoja tu (112:1).

Orodha B
A Kuteremshwa kwa Qur’an kutoka Lauh-il-Mahfudh hadi mbinguni.
B Qur’an ni neno na sheria ya Allah (s.w).
C Mfalme Abraha alikata kudhalilisha kaaba vya Waislamu.
D Makafiri walimkufuru Mtume (s.a.w) alitunga Qur’an kwa msaada wa Jibril (Mrumi).
E Udhaifu wa madai ya wapinzani dhidi ya Qur’an.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

F Qur’an inafanana na mashairi.
G Kusoma ni lazima kwa Waislamu.
H Ushahidi wa wazi kuwa Qur’an ilakutumwa na Mtume Muhammad (s.a.w).
I Msngi wa tamko la shahada.
J Malaika Jibril alileta ujumbe wa kufikisha ujumbe wa Qur’an kwa Mtume (s.a.w).
K Iblisi alimrubuni baba yetu Adamu (a.s).
L Ni muhimu kuitukuza mwezi wa Ramadhani.
M Dini ni utaratibu wa maisha unaofaa mtu.
N Siku ya malipo itamilikiwa na Allah pekee.
O Qur’an inapinga na vitendo vya viumbe waovu.

Majibu:
(i) J
(ii) E
(iii) B
(iv) M
(v) C
(vi) H
(vii) G
(viii) D
(ix) I
(x) L
(xi) F
(xii) K
(xiii) O
(xiv) N
(xv) I

3. Panga sentensi katika vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantiki. Andika herufi na namba tu zinazohusika katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Maana ya kuamini Qadar katika maisha ya kila siku huonekana kwa muumini kuwa ni mwenye kutulizana na kusubiri anapokewa na misukosuko (57:21 - 22).
(i) Wala msifurahie sana kwa alichokupeni.
(ii) Kwa yakini hii ndio ni sahihi kwa Mwenyezi Mungu.
(iii) Na Mwenyezi Mungu hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye.
(iv) Ili mshuzunike sana juu ya kitu kilichokutokeni.
(v) Hautokei msiba katika ardhi wala nafsi zenu ila umekwishandikwa katika kitabu (cha Mwenye Mungu) kabla hataujuamba.
Jibu: (v), (ii), (iii), (iv), (i).

(b) Ujasiri wa Nabii Ibrahim (a.s) wa kumlingania baba yake ambaye pia alikuwa ni kiongozi wa washirikina ni katika dalili ya kuthibitisha utume wake (19:42-46).


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

(i) (Ukifanya hivyo) utakuwa mwenziwe shetani.
(ii) Ewe baba yangu! Kwa yakini imenijia elimu isiyokujia. Basi nifuate nitakuongoza njia iliyo sawa.
(iii) Ewe baba yangu! Hakika naogoopa isije kukufikia adhabu inayotoka kwa mwingi wa rehema.
(iv) Ewe baba yangu! Kwa nini unaabudu visivyoskia na visivyoona na visivyokufaa chochote?
(v) Ewe baba yangu! Usimuabudu shetani, hakika shetani ni mwewe kumuasi mwingi wa rehema.
Jibu: (ii), (iv), (v), (iii), (i).

(c) Kutafuta elimu ni amri ya kwanza kwa mwanadamu kama tunavyojifunza katika wahyi wa kwanza kumshukia Mtume (s.a.w) (96: 1-5).
(i) Soma na Mola wako ni mkairimu sana.
(ii) Amemfundisha mwanadamu (chungu ya) mambo aliyokuwa hayajui.
(iii) Ambaye amemfundisha mwanadamu kwa msada wa kalamu.
(iv) Soma kwa jina la Mola wako aliyekuumba.
(v) Amemuumba mwanadamu kwa pande la damu.
Jibu: (iv), (v), (i), (iii), (ii).

4. Jibu maswali yafuatayo kwa kifupi kwa kuandika majibu yako katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Kwa mujibu wa Hadithi sahihi ya Mtume (s.a.w), taja mambo mawili yanayopunguza thawabu ya funga ya Muislamu.
Jibu:
i. Kusema uongo.
ii. Kufanya vitendo vya fitna au kugombana.

(b) Taja matendo manne yanayotakiwa kufanywa Hajj katika siku ya mwezi 10 Dhul-Hajj.
Jibu:
i. Kutupa mawe kwenye Jamarat.
ii. Kuchinja mnyama kwa ajili ya sadaka.
iii. Kunyoa nywele au kupunguza.
iv. Kutufu Kaaba (Tawaf Al-Ifadha).

(c) "Miongoni mwa malengo ya ndoa ni kuleta utulivu wa moyo kati ya mume na mke". Andika tafsiri ya aya inayothibitisha kauli hii.
Jibu: "Na katika ishara zake ni kwamba amekuumbieni wake zenu ili mpate utulivu kwao, na amejaalia mapenzi na huruma baina yenu." (Qur’an 30:21).

(d) Ni tofauti ipi iliyopo kati ya mtazamo wa uchumi wa Kiislamu na ule usio wa Kiislamu kuhusu dhana ya bidhaa katika biashara?
Jibu:
i. Uchumi wa Kiislamu unazingatia uadilifu na huruma katika biashara.
ii. Uchumi usio wa Kiislamu mara nyingi unazingatia faida pekee bila kuzingatia maadili.

(e) Kwa nini sera ya kudhibiti uzazi haina nafasi katika Uislamu? Taja sababu mbili.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

Jibu:
i. Uislamu unahimiza uzazi wa wingi kwa ajili ya kuimarisha jamii ya Waislamu.
ii. Kudhibiti uzazi kunaweza kuwa kinyume na agizo la Mwenyezi Mungu la kuzaa na kuongezeka.

(f) Taja sifa nne anazostahiki kuwa nazo kiongozi katika jamii ya Kiislamu.
Jibu:
i. Kuwa mcha Mungu na mwenye hofu ya Mwenyezi Mungu.
ii. Kuwa mwadilifu.
iii. Kuwa na maarifa ya uongozi.
iv. Kuwa na huruma na kuwajibika kwa jamii.

(g) Taja dalili nne za kuweza kumjua mwenye tabia ya kuheshimu watu katika Uislamu.
Jibu:
i. Kuwasalimu kwa heshima.
ii. Kuwa mkarimu kwa watu wa tabaka zote.
iii. Kutojishusha kwa maovu.
iv. Kutoa msaada kwa wahitaji.

(h) Toa maana ya istilahi zifuatazo kama zinavyotumika katika ndoa ya Kiislamu.
(i) Ijab
(ii) Kabul
Jibu:
i. Ijab: Ni kutoa pendekezo la ndoa.
ii. Kabul: Ni kukubali pendekezo la ndoa.

(i) Mtume (s.a.w) amesema, "Katika halali inayomchukiza Allah (s.w) ni talaka". Taja madhara mawili ya talaka katika jamii.
Jibu:
i. Huvuruga amani na utulivu wa familia.
ii. Huathiri malezi na maendeleo ya watoto.

(j) "Hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah (s.w)". Fafanua kauli hii katika utendaji wa maisha ya kila siku.
Jibu:
i. Kuwa na imani thabiti kwa Mwenyezi Mungu.
ii. Kufanya vitendo vyote kwa nia ya kumridhisha Mwenyezi Mungu.

(k) Taja masharti mawili ya kuthibiti kosa la zinaa katika sheria ya Kiislamu.
Jibu:
i. Mashahidi wanne waadilifu wanapaswa kushuhudia kitendo hicho.
ii. Mtu anayeshutumiwa lazima akiri mwenyewe.

(l) Ni ipi tofauti ya muda wa kukaa eda kwa mwanamke aliyeachwa na mume hali ya kuwa ni mja mzito na yule aliyefiwa na mume akiwa ana mtoto mchanga anayenyonyesha?
Jibu:
i. Mwanamke mja mzito anakaa eda hadi atakapojifungua.
ii. Mwanamke aliyefiwa na mume anakaa eda miezi minne na siku kumi.

(m) Toa fatwa kuhusu hali zifuatazo:
(i) Mtu aliyekula daku akidhani kuwa bado ni usiku lakini imeshangilia alfajiri.
(ii) Mtu aliyekula kwa kusahau katika mchana wa Ramadhani.
Jibu:
i. Funga yake itakuwa batili na atalazimika kuirudia siku hiyo.
ii. Funga yake itakuwa sahihi kwani kula kwa kusahau haina dhambi.

(n) Miongoni mwa biashara haramu katika Uislamu ni "Muzabanah" na "Muawamah". Bainisha ipi tofauti kati ya aina hizi za biashara.
Jibu:
i. Muzabanah: Ni kubadilisha matunda yanayoonekana kwa yale ya shambani kabla hayajakuzwa.
ii. Muawamah: Ni kununua mazao ya shambani ambayo bado hayajakuzwa.

(o) Andika tafsiri ya Hadithi inayoonyesha umuhimu wa kuswali sala ya jamaa msikitini.
Jibu: "Swala ya jamaa inapewa malipo mara ishirini na tano zaidi kuliko swala inayoswaliwa peke yake." (Bukhari na Muslim).

5. Chagua neno au kifungu vya maneno (i) – (xxx) ili ukamilishe sentensi (a) – (o) kwa kuandika majibu sahihi tu katika kijitabu chako cha kujibia. Maneno au vifungu vya maneno vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

(a) ________ ni miongoni mwa Waislamu walioteswa sana kwa sababu ya kusilimu kwake, lakini baadaye alikombolewa na ________.
Jibu: Bilali (r.a), Abubakar (r.a).

(b) Kusilimu kwa Omar bin Khattab kulitokana na mvuto na msisimko wa Qur’an aliosikia ikisomwa na ________ katika ________.
Jibu: Dada yake, Surat Taha.

(c) Mtume (s.a.w) alifurahisha ushauri wa ________ katika vita vya ________, ambaye alishauri kuchimbwa msingi mkubwa kuzunguka mji wa Madina ili maadui wasiweza kuwavamia kirahisi.
Jibu: Salman Alfarisy, Khandaq.

(d) Kabla ya kuletwa duniani Adam (a.s) alipewa ________ kwani ndio inayomtofautisha mwanadamu na viumbe wengine.
Jibu: Elimu.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

(e) Katika kudhoofisha Uislamu usipige hatua, wakuu wa Kikurayshi walimtishia Abu Talib ambaye hakuyumba na ndipo walipotumia mbinu ya ________ ili Mtume (s.a.w) aache kazi yake ya kulingania.
Jibu: Kuhonga.

(f) ________ ni mkataba wa Amani baina ya Mtume (s.a.w) na Makurayshi wa Makka ambao ulitokea ________.
Jibu: Hudaybia, 6 AH.

(g) Makabila makubwa ya waarabu aliyoyakuta Mtume (s.a.w) alipohamia Madina na ambayo yalikuwa na uhasama wa muda mrefu ni ________ na ________.
Jibu: Aus, Khazraj.

(h) ________ mtoto wa ________ ndiye aliyetajwa atatawala wa kifalme ambao unaenea hadi sasa katika baadhi ya nchi za kiarabu.
Jibu: Ismail (a.s), Ibrahim (a.s).

(i) Sahaba aliechaguliwa na Mtume (s.a.w) mwenyewe kuswaliisha kabla ya kufariki kwake ni ________, jambo hili lilisababisha kuchaguliwa kuwa ________ wa kwanza katika dola ya Kiislamu.
Jibu: Abubakar (r.a), Khalifa.

(j) Makka ni mji mkongwe wa kihistoria ulioasisiwa na ________ miaka mingi iliyopita wakati alipofika hapo na mkewe Hajra na mtoto wao ________.
Jibu: Ibrahim (a.s), Ismail (a.s).

(k) Mtume aliletwa ili kuwaelimisha wanadamu kuwepo kwa ________ na wake ni kigezo cha kusimamisha ________ katika jamii.
Jibu: Allah (s.w), Tawhiid.

(l) ________ ambaye alizaliwa katika utawala wa ________ wa anaijulikana kama Khalifa wa tano kutokana na mafanikio makubwa aliyoyapata katika uongozi wake.
Jibu: Omar bin Abdul-Aziz, Banu Umayya.

(m) Allah (s.w) amemleta mwanadamu hapa ulimwenguni kwa kazi moja ambayo ni ________, na alimpia ________ ili utakaomwezesha kufikia lengo hilo.
Jibu: Kumtumikia Allah, Uadilifu.

(n) Miongoni mwa njia za mapato katika dola ya Kiislamu ya Mtume (s.a.w) ni ________ ambayo ni kodi waliyopewa wasiokuwa Waislamu wanaume wenye uwezo wa kuwa askari, na ________ ni kodi waliyopewa wasiokuwa Waislamu wenye mashamba katika dola ya Kiislamu.
Jibu: Jizya, Kharaj.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

(o) Katika hatua za awali za kujenga jamii ya Kiislamu ________, Mtume (s.a.w) alianza kwa kuwafundisha waumini wake ________ ili kuweza kujenga imani zao.
Jibu: Makka, Nyenzo.



Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***